TANGAZO LA SERIKALI NA. 223 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZAO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 748 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 4(2) kwa kufuta neno "na" lililopo kati ya maneno "hayo," na "kwa".

Kufuta na kuiandika upya kanuni ya 10

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 10 na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Mazao kupoteza thamani

10. Endapo mazao yaliyokamatwa chini ya kanuni ya 9 yatapoteza thamani, Halmashauri haitawajibika kwa upotevu wa thamani kwa mazao yaliyo chini ya uangalizi wake, isipokuwa kama itathibitika kuwa upotevu wa thamani umesababishwa na Halmashauri au Wakala wake.".

Marekebisho ya Jedwali la Pili

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Pili kwa kuongeza maneno "na faini itakayotozwa na Mkurugenzi baada ya kukiri kosa" mara ya maneno "ushuru ninaodaiwa".

Dodoma,
10 Januari, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*